



## Uchambuzi wa Bajeti ya UKIMWI 2009/2010: Tunaelekea Wapi?

Kwa kupitia nyaraka mbalimbali zilizoandaliwa na serikali, uchambuzi huu unalenga kuangalia mgawanyo wa fedha za UKIMWI kwa mwaka 2009/2010 ili kuwataarifu wadau mbalimbali kuhusu mwelekeo wa taifa katika juhudu zake za kupambana na suala mtambuka la UKIMWI.

Katika mwaka 2009/2010 wa fedha, bajeti ya taifa imeongezeka kwa takriban asilimia 31 kutoka shilingi trilioni 7.5 mwaka 2008/2009 wa fedha hadi shilingi trilioni 9.5 mwaka huu. Lakini ongezeko hili la fedha halijaakisiwa katika bajeti ya UKIMWI. Kati ya taasisi zote ambazo fedha za bajeti ya UKIMWI huelekezwa – Serikali Kuu, Serikali za Mikoa, Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) – ni Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI peke yake ambao umeongezewa fedha katika mwaka 2009/2010 wa fedha.

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI imetengewa asilimia 68 ya bajeti nzima ya UKIMWI, au shilingi bilioni 103.1, ambayo ni ongezeko la asilimia 113 kutoka mwaka 2008/2009. Hii inaashiria kuwa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI unategemewa kuwa mwendeshaji mkuu wa kampeni dhidi ya UKIMWI mwaka 2009/2010.

Bajeti ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI kwa upande wake, kinyume na ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, imepungua kwa asilimia 34 kutoka mwaka 2008/2009. Katika matumizi yake ya fedha mwaka huu, Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI inaonekana kujikita zaidi katika kutimiza malengo ya MKUKUTA. Kati ya bajeti nzima ya mwaka huu wa 2009/2010 wa fedha, Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI imeelekeza asilimia 91.3 ya bajeti yake yote, ya bilioni 26.6, sawa na shilingi bilioni 24.3, moja kwa moja katika shughuli za MKUKUTA.

Kwa upande wa ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka 2007/2008 wa fedha:

- Halmashauri 72 kati ya halmashauri 133 zilizokaguliwa, au asilimia 54, zilipata **hati zinayoridhisha**; ukilinganisha na mwaka 2006/2007 wa fedha ambapo halmashauri 100, au asilimia 81, zilipata hati zinazoridhisha; na
- Halmashauri 61 kati ya 133 zilizokaguliwa, au asilimia 46, zilipata **hati zenye shaka**; ukilinganisha na mwaka 2006/2007 wa fedha ambapo halmashauri 24, au asilimia 19, zilipata hati zenye mashaka.

Mapendekezo ya uchambuzi hii ni kuwa:

- Juhudi za uelekezaji rasilimali katika halmashauri ni lazima ziende sambamba na juhudi za kuwajengea uwezo watendaji katika ngazi hii;
- Shughuli za VVU/UKIMWI zinahitaji kujumuishwa katika miradi na mikakati mbalimbali ya kiuchumi ukiwemo Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA);
- Kuwepo na uwazi zaidi na upatikanji wa vitabu vya bajeti katika muda unaofaa ili uchambuzi uweze kufanyika mapema na kuwezesha matokeo yake kuchangia katika mijadala ya bajeti.



*Taarifa zaidi juu ya ripoti hii inapatikana katika tovuti yetu:*  
[www.yav.or.tz](http://www.yav.or.tz)